# Uhuru na Amani

GAZETI LA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA TOLEO LA 1, 2016 Bei Sh. 1,000/-




**NDANI:**

- Maono yatakupa maendeleo
- Tuache fikra mgando
- Katibu Mkuu LWF atembelea KKKT



Vol. 116, Toleo la 1, 2016

ISSN 0856 - 1214


Moshi Lutheran
Printing Press
Tunachapisha:
Vitabu vya aina zote
Majarida na Magazeti
Hati za Fedha
Madaftari
Bahasha
Vipeperushi
Tiketi za vyombo vya Usafiri
Mabango ya matangazo
kadi za Kila aina
Pia tunatoa huduma za:
Type Setting na Usanifu
Ukarabati vitabu Chakavu
Wasiliana nasi:
Moshi Lutheran Printing Press
S.L.P 301, Moshi
Kilimanjaro
Simu: +255 272 750 546
Mob: +255 752 327 899
Moshilutheranpress@gmail.com

**Uhuru na Amani**
Gazeti la KKKT
**Toleo la 1, 2016**
Vol. 116 Na. 1
**ISSN 0856 - 1214**

# MAONI YA MHARIRI

Kwa muda mrefu watendaji katika Ofisi za umma walikuwa wamejenga tabia ya kutowajibika, ubadhirifu wa mali ya umma na baadhi yao kula njama kwa kushirikiana na wakwepa kodi ili wapate rushwa na kusababisha Serikali isipate mapato yanayotakiwa kwa mujibu wa sheria.

Baadhi ya watendaji waliacha kuwahudumia au kutatua matatizo ya wananchi na badala yake walitumia vyeo vyao kudai rushwa; kujichukulia marupurupu, posho nyingi za vikao na posho kubwa za safari za ndani na nje ya nchi.

Alipoingia madarakani na kuanza kwa kulihutubia Bunge mwezi Novemba mwaka jana, Rais wa Awamu ya Tano, Dkt. John Pombe Magufuli, alirudia ahadi aliyoweka wakati wa kampeni ya uchaguzi kwamba atajihusisha kikamilifu kurejesha uwajibikaji katika sekta ya umma, kupambana na rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma.

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) lilichukua fursa wakati wa kuingizwa kazini Mkuu wa Kanisa wa Awamu ya Tano, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo, kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla kwa kuanzisha operesheni ya kupambana na ubadhirifu wa mali za umma na rushwa.

Mkuu wa KKKT, alitoa wito kwamba Serikali iwe makini katika kutekeleza operesheni hiyo inayojulikana kama: "utumbuaji majipu". Alisema Serikali chini ya uongozi wa Rais Magufuli imejizolea sifa toka watu wengi duniani kote kwa kuongoza vita hiyo.

Askofu Dkt. Shoo alisema hayo mbele ya watu wapatao 5,000 waliohudhuria ibada hiyo wakiongozwa na Waziri Mkuu wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa, aliyewakilisha Serikali katika ngazi ya kitaifa.

Askofu alitoa mfano wa mtu aliyekuwa na wivu na kaka yake hivyo akamdanganya baba yao kwamba kaka anajipu. Na baba alilitumbua na kumwachia jeraha kubwa kwa kuwa lilikuwa si jipu bali ni kipele tu. Hivyo akasema operesheni inayoendelea nchini ya 'kutumbua majipu' (kupiga vita ubadhirifu na rushwa) ifanywe kwa uangalifu mkubwa ili watu wenye nia mbaya wasitumie jambo zuri kama hilo kuwaonea wenzao. Alisema "ubinafsi ndio uliotufikisha hapa" na akarudia kumpongeza rais kwa hatua za kurekebisha maovu katika jamii ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanisha na "majipu".

Katika operesheni hiyo baadhi ya viongozi wa vitengo nyeti na mashirika makubwa ya umma wameondolewa au kusimamishwa kazi mara moja ili kupisha uchunguzi wa tuhuma hizo.

Kutokana na opereshini hiyo, kwa muda mfupi Serikali imetangaza makusanyo ya kodi kuongezeka na baadhi ya sekta muhimu zimekwishapewa mgao wa fedha zilizookolewa kutokana na kodi ambayo haikuwa imekusanywa siku za nyuma.

Hizo ni jitihada za dhati za Serikali katika kuhakikisha kwamba watendaji wanatimiza kauli mbiu ya "hapa kazi tu" kwa kuwajibika kwa kutoa huduma kikamilifu, kurejesha nidhamu, kuondokana na ubadhirifu na rushwa.

Tunachosubiri ni mikakati na mipango thabiti ya utekelezaji; mabadiliko ya sheria na sera kuendana na mwelekeo mpya wa Serikali na uimarishwaji wa mfumo wa utendaji ili hayo yote mazuri yawe endelevu. Mungu ibariki Tanzania.

Uhuru na Amani ni Gazeti la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Hutayarishwa na Kitengo cha Mawasiliano, KKKT.

Maoni yaliyomo katika makala zinazochapishwa ni ya mwandishi anayehusika na wala hayawakilishi mawazo ya Kanisa ama mhariri isipokuwa pale ambapo imetamkwa wazi.

Ukiwa na maoni, ushauri, makala au maswali mwandikie:
**Mhariri**
**Uhuru na Amani**
**S.L.P. 3033**
**ARUSHA**
**Barua pepe:** elobulu@elct.or.tz
**Sms** Whats App kwa Mhariri: +255-754-482-285
**Fungua Tovuti ya KKKT:**
http://www.elct.org/

**MHARIRI**
**Elizabeth Lobulu**

Limepigwa Chapa na:
**Moshi Lutheran Printing Press**
S.l.P 301 Moshi
lutheranpress@yahoo.com

**Newspaper Design & Typesetting:**
**Elizabeth Lobulu**

**Wachangiaji wa Makala:**
Mchg. Dkt. Martin Junge
Dkt. Hellen Kijo-Bisimba
Patricia Mwaikenda
Shemeji Melayeki
Pauline Kimollo
Mch.Thomas Maumbuka
Anna Mahenge

**Wachangiaji Picha:**
Michael Shayo, KKKT DK
Ibrahim Maguru, KKKT DK
Jari Berg, FELM

**PICHA YA JALADA:**

Mkuu wa Kanisa, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo, akimpa Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, zawadi baada ya Askofu Shoo kuingizwa kazini kuwa Mkuu wa KKKT huku Mkuu wa Kanisa wa Awamu ya Nne, Askofu Dkt. Alex Malasusa, akishuhudia.

Picha ya pili ni Kwaya ya KKKT Usharika wa Moshi Mjini.

(Picha na Michael Shayo, KKKT DK)

# Junge afanya ziara KKKT



Mchg. Dkt. Martin Junge akitia saini kitabu cha wageni akiwa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

**Na Elizabeth Lobulu**

Katibu Mkuu wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD), Mchg. Dkt. Martin Junge, alifanya ziara ya siku mbili nchini kwa mwaliko wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Alianza kwa kutembelea Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (TUMA) na alikutana na Maaskofu na viongozi wengine wa KKKT tarehe 30 Jan 2016. Alikwenda Chuo Kikuu hicho cha KKKT akifuatana na Katibu wa Afrika wa FMKD, Mchg. Dkt. Elieshi Mungure na Katibu Mkuu wa KKKT Bw. Brighton Killewa.





Lango la ofisi mpya zilizo pamoja na Ukumbi wa mikutano.

Lengo lilikuwa kuonana na uongozi na wahadhiri wa Kitivo cha Theologia na kuzuru baadhi ya maeneo ya chuo ukiwemo ukumbi wa mikutano, kumbi za mihadhara na mabwalo mawili ya chuo.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Profesa Joseph Parsalaw, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Utawala), Mch. Dkt. Faustin Mahali na Mkuu wa Kitivo cha Theologia, Mchg. Dkt. Anjela Olotu walikuwa miongoni mwa viongozi waliofanya naye mazungumzo.



Mchg. Dkt. Martin Junge, Katibu Mkuu wa FMKD, akiongea na Wakufunzi wa Theologia alipokuwa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira hivi karibuni.



Baadhi ya wanafunzi wakifanya kazi ya kikundi wakati Katibu Mkuu wa FMKD alipotembelea Chuo cha Tumaini Makumira hivi karibuni.

# Tushirikishane na kupanga pamoja

Akiwaeleza Maaskofu wa KKKT kuhusu maadhimisho ya miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa, Mchg. Dkt. Junge alirejea mazungumzo yake alipokuwa TUMA kwa kutaja mambo matatu muhimu.


Mosi, ni kutokana na ***Matengenezo*** ndiyo maana Kanisa limeweza kuenea dunia nzima na kila Msharika pale alipo ana mchango utakao liendeleza Kanisa.

Pili, katika safari ya kuendea maadhimisho ya miaka 500 ya ***Matengenezo ya Kanisa*** inabidi jumuiya ya FMKD ihoji tulipokosea ili kujirekebisha na kuombana msamaha kwa makosa yetu.

Na ndio sababu alisema, Oktoba mwaka huu (yeye) Mchg Junge, Rais wa FMKD, Askofu Munib Younan na Mkuu wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Fransis, watashirikiana kuandaa na kuwa wenyeji wa mkutano wa pamoja kutathmini miaka 50 ya majadiliano baina ya Kanisa la Kilutheri na Kanisa Katoliki hasa kuelekea kilele cha ***Matengenezo*** 2017.

Lengo ni kuondoa hali ya uhasama na kuelekeza nguvu kwenye ushirikiano zaidi, alieleza Katibu Mkuu huyo wa FMKD. Jambo la tatu ni kutafakari mahali tulipo kama jumuiya na mambo ya kufanya siku zijazo. Akasema KKKT ambalo ni kanisa la tatu kwa ukubwa katika FMKD, linategemewa kutoa mchango wake kwa kuendelea kutoa ushirikiano katika safari hii kuelekea 2017. Alirudia tena kushukuru KKKT kwa kuendelea kumhudumia mwanadamu kiroho, kimwili na kiakili.

**Akiwa katika ukumbi wa mikutano, Dkt. Junge alikuta wanafunzi kutoka shule nane za Sekondari zilizopo karibu na TUMA wakishiriki katika mashindano ya ngoma za asili yaliyoandaliwa na Kituo cha Utafiti, Utamaduni na Sanaa (Culture and Arts Centre) ambacho ni sehemu ya Chuo. Kwa maelezo zaidi fungua tovuti ya TUMA: www.makumira.ac.tz**



# Kanisa lapongezwa kwa kubadilisha uongozi kwa amani

Alipofanya mazungumzo na viongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) tarehe 30 Januari 2016, Katibu Mkuu wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD), Mch. Dkt. Martin Junge, alipongeza KKKT kwa hulka ya kubadilisha viongozi kwa amani; hali ambayo alisema inadhihirisha kwamba Kanisa limekuwa.



Katibu Mkuu wa FMKD, Mchg. Dkt. Martin Junge, akizungumza na viongozi wa KKKT. Mazungumzo hayo pia yalihudhuriwa na Maaskofu na wawakilishi wa Mashirika ya Misioni toka Ulaya na Marekani.

Pia alilishukuru Kanisa kwa kuwa na mchango mkubwa wa hali na mali katika jumuiya ya FMKD.

Alisema hakuna kanisa kubwa lisilohitaji msaada toka kwa wengine na hakuna kanisa dogo ambalo halina mchango kwa wengine.

Mch. Dkt. Junge ambaye alikuwa katika ziara ya siku mbili nchini, alitembelea Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (TUMA) na kuhubiri katika Ibada ya kumwingiza kazini Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo.

## SIKU YA MAOMBI YA DUNIA

# Nyenyekeeni na kutenda haki - wito



Mchg. Anna Makyao

Watumishi wa Ofisi Kuu ya KKKT waliadhimisha Siku ya Maombi ya Dunia tarehe 4 Machi 2016 kwa Ibada maalumu iliyoandaliwa na Kurugenzi ya Wanawake. Akihubiri siku hiyo **Mchg. Anna Makyao** alitumia Somo kutoka Injili ya Marko (Sura ya Tisa na ya 10) kuhusu wanafunzi wa Yesu walivyozuia watoto wadogo wasimsogelee Yesu, (Marko 9: 36 - 37). Endelea kusoma alichosema:

Yesu aliona nini kwa watoto hadi aseme atakayempokea mtoto mmoja kati ya hawa ampokea Yeye? Tunajifunza nini kutoka kwa watoto? Na tujihoji tunaenendaje katika ulimwengu ambapo watoto wananyanyaswa pamoja na makundi ya wazee wanaodhalilishwa?

Watoto ni walimu wazuri katika kujifunza unyenyekevu, kusamehe, kutohesabu mabaya na kuweza kuishi pamoja na watu wengine. Yesu akijibu swali la wanafunzi kwamba ni nani aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni, ***"Akatwaa kitoto, akamweka katikati yao, akamkumbatia, akawaambia: Mtu akimpokea mtoto mmoja wa namna hii kwa jina langu, anipokea mimi; na mtu akinipokea mimi humpokea si mimi, bali Yeye aliyenituma,"*** (Marko 9: 36 -37). Kundi hili la Kiyahudi liliangalizwa jinsi inavyopaswa kuwa. Linaitwa liwe na tabia kama ya watoto.

Wazazi walifurahi jinsi Yesu alivyowatendea watu mambo mema na wakatamani wawapeleke watoto kwa Yesu ili awaguse. Wanafunzi walipowakemea wazazi, Bwana Yesu alichukizwa na jambo hilo akasema: ***"Waacheni watoto waje kwangu, msiwazuie; kwa maana watoto kama hawa ufalme wa Mungu ni wao".*** Watoto wanahitaji kupendwa na kuheshimiwa. Watoto wakilelewa katika hali hii basi wao wenyewe wanafurahi na ni baraka kwa watu wote. **Maombi ya Dunia** mwaka 2016 yanaangaliza kuwajali watoto na kuwa tayari kuwaangalia watu wote na kuwatendea mema.

Tuwaruhusu watoto waguswe na Yesu. Na tunapaswa kutubu kwa jinsi ambavyo tumewazuia watoto kuguswa na Yesu na kwa kufanya hivi tumewanyima haki zao. Kwa mfano Ibada za Watoto hazifanyiki ipasavyo. Vifaa vya Ibada za watoto havinunuliwi na hii inaonesha hatuwatendei haki. Watoto wengi kwa ujumla wanafanyiwa vitendo vya ukatili.

Tuwapeleke watoto kwa Yesu nao watakuwa raia wema katika dunia yetu na ili waweze kupata matumaini. Tujifunze kwa Yesu na kujihoji: 'Nimechangia kiasi gani kufanya ukatili kwa watoto?'

Yapo makundi mengine ambayo tumeyazuia yasiguswe na Yesu na kuyaona hayafai kukaa na Yesu. Hawa ni wale waliotengwa na kuonekana hawafai kwa mfano watoto walemavu ambao hawana msaada. Jamii huwaona watoto walemavu kama mkosi au laana. Hawapati nafasi ya kwenda shule. Je kama Kanisa tunawasaidiaje au tuna mchango gani kuwasaidia watoto wanaohitaji msaada?

Nimetumikia kwa miaka 25 katika Kanisa kama Mchungaji, lakini nimeona wapo wakuu wa jimbo wachache



**Bibi Faustina Nillan, Mkurugenzi wa Kazi za Wanawake na Watoto, KKKT aliyeandaa Ibada ya Siku ya Maombi ya Dunia Ofisi Kuu ya Kanisa.**

wanawake lakini sijaona Msaidizi wa Askofu mwanamke. Je ni kwamba hakuna mwanamke aliye na uwezo au tumewazuia kwenda kwa Yesu?

Katika Sharika nyingi mwanamke ndiye anayerudishwa kundini kwa kuzaa nje ya ndoa lakini mwanaume harudishwi wala kuulizwa lo lote kuhusu jambo hilo. Somo la **Siku ya Maombi ya Dunia** litufungue ili tuwe tayari kuwapokea, kuwasaidia na kuwaleta katika uwepo wa Mungu wale walio nje. Kwa kufanya hivyo ni kumpokea Bwana Yesu alipokuwa na njaa, kiu, alipokuwa uchi, nk.

Hivi karibuni mwanamke katika Usharika wa Pasua alimwandikisha mtoto Antony kwa ajili ya Shule ya Chekechea. Kumbe mtoto huyo alikuwa na shida ya mfumo wa kutoa uchafu mwilini ambapo zilitakiwa sh. 700,000 za operesheni na mzazi hakuwa na uwezo na ameishi naye kwa miaka saba katika mazingira magumu sana ya malezi. Je tukisikia hayo tunakuwa tayari kuchangia? Mbona tuko tayari kuchangia harusi na ubarikio lakini si kusaidia wahitaji?

Wasiliana na Mchg. Anna Makyao kwa sms: +255 759 205 043

# Mfumo wa kukusanya takwimu watathminiwa

Programu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TEHAMA inayoendeshwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kwa lengo la kuboresha ukusanyaji, utunzaji na utoaji taarifa za wagonjwa katika hospitali kwa kutumia mfumo wa kisasa wa komputa unaojulikana kama Care2x utafanyiwa tathmini mwezi Aprili - Juni 2016, ambapo ni miaka 10 sasa tangu ulipoanza kutumika katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya hapa nchini.

Finnish Christian Medical Society (FCMS) pamoja na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela ndiyo wadau watakaofanya tathmini hiyo. Mfumo huu wa kompyuta unatumika katika hospitali za Arusha Lutheran Medical Center (ALMC) inayo julikana kama Hospitali ya Selian ya mjini Arusha, KKKT; Hospitali ya Kilutheri ya Haydom na Hospitali ya St. Elizabeth (Katoliki). Hospitali nyingine zinazonufaika ni Hospitali ya Rufaa Mbeya; Hospitali ya Taifa ya Tiba ya Akili Mirembe, Dodoma; Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ya Kuambukiza, Kibong'oto;na Hospitali Teule ya Halmashauri ya Makiungu (Katoliki). Lengo la tathmini ni kujua kwa kiasi gani mfumo wa Care2X unakidhi haja ya watumiaji wakati ambapo program ya TEHAMA ya KKKT inajipanga kunufaisha hospitali nyingi zaidi. Mwezi Novemba 2015 watumishi wa program ya TEHAMA walishiriki mafunzo ya kujenga uwezo wa kuboresha mifumo ya takwimu za afya yaliyoandaliwa na FCMS na Chuo Kikuu cha Tampere, Finland. Mwezi Machi 2016 Bi Kristina Nokso-Koivisto toka FCMS alifika Ofisi Kuu ya KKKT na kukabidhi vyeti vya kufuzu mafunzo hayo.



**Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti KKKT, Mchg. Lazaro Rohho, akimpongeza Bw. Martin Elistante na Bibi Pauline Kimollo Machi 2016 mwaka huu walipotunukiwa Vyeti na Chuo Kikuu cha Tampere, Finland vya Mafunzo ya Care2X. Wa pili kulia ni Bi. Kristina Nokso-Koiviosto aliyetoa vyeti hivyo. Yeye ni Meneja wa Mradi huo kutoka chama cha** Finnish Christian Medical Society**.**

# Harakati za kupinga ukatili

Harakati za kupinga vitendo vya ukatili zimezinduliwa rasmi kwa watumishi wa Ofisi Kuu ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) hivi karibuni. Bi Eva Palmqvist (pichani kushoto) ambaye ni Afisa Ushirikiano wa Kanisa la Sweden aliye Ofisi Kuu ya KKKT, alisema wanaounga mkono harakati hizo zilizoanzishwa na Baraza la Makanisa Duniani (WCC), kila Alhamisi huvaa nguo nyeusi na beji kama ishara ya kuunga mkono jitihada za kujenga jamii yenye haki na amani na isiyo na hofu ya ukatili.

Wakati wa uzinduzi huo, Bi Anna Mahenge (pichani kulia) toka Kitengo cha Huduma ya Tiba Shufaa, alisema 'kwa kukubali kushiriki harakati hizo tuanze kubadilika wenyewe na mbegu iliyopandwa leo ichipue baadaye ili kuwabadilisha wengine.' Alisema tupige vita ukatili tangu ngazi ya familia ili kuwa chachu ya mabadiliko.



# Kanisa la Marekani lachangia SUN Sekondari

Usharika wa 'Prince of Peace' uliopo Minnesota, Marekani umechangia Dola za Kimarekani 41,500 kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Ushirika wa Neema (SUN) iliyopo Mpanda. Kati ya fedha hizo, Dola za Kimarekani 32,000 zilichangwa kwa heshima ya kuingizwa kazini Mkuu mpya wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo mnamo 31 Januari 2016.

Shule ya SUN ni mali ya KKKT Dayosisi ya Kaskazini.



**Bw. Munguatosha Makyao, Mkuu wa Idara ya Hazina KKKT Dayosisi ya Kaskazini.**

Mkuu wa Idara ya Hazina KKKT Dayosisi ya Kaskazini, Bw. Munguatosha Makyao, alimwandikia barua hivi karibuni Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa 'Prince of Peace', Chad Brekke; akishukuru Mungu kwa kuonesha urafiki wa kweli na kwa kujitoa kwao kusaidia walio wahitaji katika jamii. Na aliongeza kuwa, Dayosisi itazidi kufanya maombi kwa ajili yake, mshirika wao anayeitwa Bw. Ed McNulty, na kwa ajili ya watu wa Marekani.

# WIKI YA MAZINGIRA

## Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania

**28 Februari - 5 Machi 2016**

# Chuo cha Kidugala chaanzisha somo la 'Theologia ya Kijani'

**Na Patricia Mwaikenda**

Dayosisi ya Kusini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) imeanzisha Mradi mahsusi wa Kuhifadhi Mazingira unaoitwa "Theologia ya Kijani" katika Seminari ya Kidugala, Njombe. Kutokana na elimu wanayopata toka Chuo cha Biblia Kidugala wanafunzi wanaonesha ubunifu mkubwa hasa katika utunzaji wa mazingira na kuyaweka katika hali ya kuvutia wageni wanaofika chuoni hapo.

Ili kuhakikisha utunzaji wa mazingira unakuwa sehemu ya mafunzo katika kituo hicho mtaala wa "Theologia ya Kijani" uliandaliwa rasmi na Dayosisi.

Wanafunzi wanajifunza utunzaji wa mazingira kwa nadharia na vitendo. Chuo kinaendesha mambo ya kilimo, mazingira na utalii (agric- ecotourism).

Chuo kinawapa fursa wanafunzi kuonesha vipawa vyao katika kubuni vivutio vinavyoweza kuendana na utunzaji wa mazingira ili wageni mbalimbali wanapotembelea chuo na mazingira yake wajifunze kilimo rafiki kwa mazingira, waone msitu wa Kidugala na maporomoko ya maji.

Pamoja na kutunza mazingira kazi ya kilimo inakipatia chuo faida nyingi.

Seminari ya Kidugala imepanda aina mbalimbali za mazao ikiwepo miti ya matunda na migomba.

Bustani ya mboga yenye ukubwa wa ekari mbili imepandwa bilinganya, ngogwe, kabichi, spinachi, nk. Chuo kimepanda pia vitunguu.

Chuo kinatumia wakai wote mbolea ya wanyama kama ng'ombe, nguruwe, kuku na simbilisi katika kilimo. Wanyama wote hao wanafugwa chuoni.

Katika kuhakikisha msitu wa Kidugala unahifadhiwa, chuo kimeanzisha upandaji wa miti ya asili na kuzuia uchungaji wa makundi makubwa ya ng'ombe katika msitu ambayo huchangia uharibifu wa mazingira.

Pia chuo kimezuia shughuli za kilimo kwenye vyanzo vya maji, ukataji miti na uchomaji moto katika msitu wa Kidugala.

Uanzishwaji wa kitalu cha miti umeongeza kasi ya upandaji miti katika maeneo mbalimbali ya chuo. Chuo cha Kidugala kina mabwawa kadhaa ya samaki aina ya tilapia/ perege. Kazi zote hizo zinafanywa na wanafunzi kwa ushirikiano na warumishi.



**Askofu Mengele wa KKKT Dayosisi ya Kusini akipowaongoza wageni waalikwa wa Mkutano Mkuu wa XXI wa Sinodi ya Dayosisi ya Kusini kutembelea Mradi wa mazingira Chuoni Kidugala.**



**Utunzaji wa Mazingira ni sehemu ya mafunzo wanayopata wanafunzi wa Chuo cha Seminari Kidugala.** (Picha na Patricia Mwaikenda)



# Seminari ya Kidugala kuwa kivutio cha utalii

Seminari ya Kidugala inatoa mafunzo kwa Wachungaji, Wainjilisti na Walimu wa Muziki. Chuo kinatoa Astashahada ya Theologia kwa Wachungaji.

Pamoja na kusoma theolojia wanafunzi wa Seminari wanachukua masomo ya Sekondari na ujasiriamali.

Na kama ilivyoelezwa awali Somo la Theologia ya Kijani (hasa kutunza mazingira) ni sehemu ya masomo ya Theolojia chuoni hapo. Ni matumaini ya chuo kuwa endapo msitu wa Kidugala na mazingira yake yatahifadhiwa itakuwa nafasi ya pekee wageni toka maeneo mbalimbali kufika na kutizama uumbaji wa Mungu. Pia wageni watapata nafasi ya kuona kazi mbalimbali zinazo tekelezwa na chuo.

Dayosisi ya Kusini ni miongoni mwa Dayosisi zilizo mstari wa mbele katika kutunza uumbaji na kuhifadhi mazingira kwa ujumla.

Dayosisi inamiliki mashamba ya miti maeneo mbalimbali kwa mfano Shamba la Miti Mgala lenye ukubwa wa ekari 55 na Shamba la Miti Ngengedu lina ekari 50.



**Chuo kinazuia uharibifu wa mazingira katika misitu na vyanzo vya maji.**

**Wasiliana nao kwa barua pepe:**
**kidugalaseminary@yahoo.com au**
**elikanalova@yahoo.co.uk au**
**rev.mexon@gmail.com**

# Tumtazame Mungu ili kutunza mazingira

**Na Mchg. Thomas Maumbuka**

**Utangulizi:**

**Ni jukumu la Nani kutunza mazingira?**

***"Bwana Mungu akamtwaa huyo mtu akamweka katika bustani ya Edeni ailime na kuitunza,"*** (Mwanzo 2: 15).

Mazingira yana mchango mkubwa katika afya ya mwanadamu maana kuna uhusiano wa mti na mwanadamu. Mstari wa 29 tunasoma: ***"Tazama nimewapa kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi".*** Baada ya kupewa bustani tumeitumia vibaya kwa kuharibu badala ya kutunza.

Nimetembelea *Mbuga za Wanyama* kadhaa hapa nchini kama vile *Ngorongoro, Tarangire, Manyara, Serengeti na Mikumi.* Katika maeneo hayo mazingira yanatunzwa vizuri sana, ndiyo *'Eden'* anayoisema Mungu. Kuna aina mbalimbali za wanyama, ndege na maji ya kutosha. Hivyo ni kivutio kwa watalii na ndio sababu wameweka tozo ya lango ukifika unalipia ada kwa kupita katika mbuga. Hata hali ya hewa ni tofauti maana jua linapoozwa na misitu.

Macho yetu hayamtazami Mungu ndio maana uharibifu huu umeongezeka. Kwa mfano katika Wilaya ya Kishapu,



**Mchg. Thomas Maumbuka**

Shinyanga kuna ukame sana. Kutotunza mazingira kunaharibu pia imani, upendo, furaha, afya, nk.

**Jinsi ya kutunza mazingira**

Rais wa awamu ya tano aliagiza watu wasafishe mazingira na watu wakatoka kwa wingi kufanya usafi wa maeneo yao na maeneo mengine kama masokoni, hospitalini na katika barabara za mijini. Lakini tusingoje mpaka hali iwe mbaya ndipo mtu atukumbushe kutunza mazingira.

Yapo mambo matano yanayoweza kusaidia uweze kutunza mazigira. Jambo la kwanza, tukubali siku zote kuwa tayari kupokea wajibu wa kutunza mazingira ya kimwili na kiroho.

Pili tujiandae kwa wajibu huo kwa mfano Musa aliandaliwa alipoambiwa ***"vua viatu"*** vyako kabla ya kupewa wajibu wa kuwakomboa wana wa Israeli. Daudi kabla ya kupambana na Goliathi aliandaa kombeo na hata Esta alifunga na kuomba kwa ajili ya watu wake.

Tatu inabidi kutambua kwamba ziko changamoto utakazo kumbana nazo lakini wewe umtazame Bwana wala usiogope. Fanya uliyojipangia kufanya kwa bidii. Usimwangalie mtu, mtazame Bwana. Jambo la nne ni kuwa tayari kulipa gharama. Mfano, Musa alifika mbele ya Farao na kumwambia awaache wana wa Israeli waondoke bila kuogopa kwamba angeweza kufa. Esta aliingia kumwona Mfalme kinyume na utaratibu na hakujali kwamba angeweza kuangamia. Wote hawa walimtazama Bwana hata kama mazingira ya uhai wao hayakuwa salama.

**Hitimisho**

Na jambo muhimu kuliko yote ni ku unataka kufanya nini na uweke mpango kama vile kupanda miti, kufanya usafi wa mazingira, kuhimiza wengine wapande miti na mwisho ujipime katika hayo.

**Wasiliana na Mchg. Thomas Maumbuka kwa sms:**
**0768 424 408**

# TOLEO MAALUMU

## Mkuu wa KKKT Awamu ya 5 aingizwa kazini

# Watumishi toeni huduma, acheni ubinafsi - Mkuu KKKT

**Na Elizabeth Lobulu**

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo, amewataka watumishi wa Kanisa barani Afrika watoe huduma waliyoitwa kufanya na kuacha ubinafsi kwani uongozi ni utumishi.

Alisema hayo kama sehemu ya itikio lake mara baada ya kuingizwa kazini kuwa Mkuu wa KKKT, Awamu ya Tano, katika Ibada iliyofanyika Kanisa Kuu la Kilutheri, Usharika wa Moshi Mjini, 31 Januari 2016.



**Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo, akitambulishwa kwa washarika mara baada ya kuingizwa kazini na Mkuu aliyemtangulia, Askofu Dkt. Alex Malasusa (kushoto).**

Aliwaambia waliohudhuria ambao ni pamoja na viongozi wa makanisa wawakilishi wa jumuiya za Kikristo ndani na nje ya nchi kwamba watumishi wa Kanisa barani Afrika hawana budi kujitoa kweli kwa kuwa utumishi ni dhamana. Alisema viongozi watekeleze wajibu wao na siyo kuwa wabinafsi kwa kutumia nafasi zao kujitajirisha binafsi. Alisema sasa wakati umefika tupige vita ubinafsi uliokithiri.



**Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa akiwa na viongozi wa Kanisa. Aliyeshika Fimbo ni Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Shoo** (Picha na Ibrahim Maguru KKKT DK).



**Mkuu wa Kanisa aliyemaliza muda wake, Askofu Dkt. Alex Malasusa (kulia), aliongoza Ibada kwa kusaidiwa na Askofu Solomon Massangwa.**



**Maandamano yalianzia Hosteli ya Umoja hadi Kanisa Kuu la Kilutheri Dayosisi ya Kaskazini, Usharika wa Moshi Mjini.**



**Baada ya Mkuu kuingizwa kazini, pamoja na mambo mengine alimwingiza kazini Bibi Alice Mtui Kyaruzi kutoka Dayosisi ya Konde kuwa Mwandishi wa KKKT.**

**Watu wapatao 5,000 wakiwemo washarika, viongozi wa Kanisa toka ndani na nje ya nchi, viongozi wa Serikali, wanasiasa kwaya za kawaida na za tarumbeta toka ndani na nje ya nchi zilishiriki katika Ibada. Kundi la watu 17 la Kwaya ya Tarumbeta lilitoka Ujerumani.**

# Waziri Mkuu apongeza KKKT

Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa, amelipongeza Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kwa kuwa mdau wa maendelo kwa kutoa huduma mbalimbali za kijamii nchini.

Alisema hayo alipokuwa mgeni rasmi kutoka upande wa Serikali katika Ibada ya kumwingiza kazini Mkuu mpya wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo, iliyofanyika Moshi, 31 Jan. 2016.

Alisema kwa idadi ya vituo vya huduma za jamii karibu 600 vilivyoko katika Dayosisi ya Kaskazini peke yake Kanisa lina uzoefu; hivyo milango ya Serikali iko wazi kupokea ushauri kutoka kwa Mkuu wa KKKT wakati wo wote.

Waumini walishangilia aliponukuu kutoka Kitabu cha 1 Timotheo 3: 1 kuhusu wajibu wa Askofu. Na baada ya kusoma, alisema Mkuu mpya wa KKKT anazo sifa zote zilizoorodheshwa. Aliongeza kusema kwamba Serikali itawashirikisha wadau wa elimu kujadili ada elekezi zilizo pendekezwa hivi karibuni. Aliahidi kufikisha Serikalini maoni ya Kanisa kwamba mihimili ya dola isiingiliane na alikumbusha umuhimu wa kuwa makini katika kampeni ya kupiga vita ufisadi na ubadhirifu nchini.



Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, akihutubia wakati wa Ibada ya kuingizwa Kazini Mkuu mpya wa KKKT. Kanisa linaunga mkono jitihada za kupiga vita rushwa na ufisadi na limeahidi kuendelea kuombea viongozi wa Serikali.




Askofu Dkt. Heinrich Bedbord-Strohm kutoka Muungano wa Makanisa ya Kiinjili ya Kilutheri Ujerumani alitoa salamu kwa niaba ya viongozi wa Makanisa na Vyama vya Misioni vya Ulaya na Marekani. Walihudhuria maaskofu 28 toka ndani na nje ya nchi.



Msaidizi wa Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini, Mchg. Elingaya Saria akimpongeza Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo ambaye pia ni Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini.



Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa, akisalimiana na Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa.



Katibu wa LMC, Bw. Peter Karlsson alipewa nafasi kutoa salamu wakati wa hafla ya chakula cha mchana iliyofanyika Uhuru Hotel baada ya Ibada.

## Kanisa si kampuni ya mtu binafsi

Kabla ya kumkaribisha Waziri Mkuu kuongea, Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Shoo alisema hapa Tanzania Kanisa ni mdau wa maendeleo na siyo kampuni ya mtu binafsi. Alisema hapa duniani Kanisa ni moja na tena lina mwenyewe ambaye ni Bwana wetu Yesu Kristo. Na lina wajibu wa kumhudumia mwanadamu kikamilifu kiroho, kimwili na kiakili.



Wasaidizi wa Maaskofu wakiandamana.



Katibu Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini, Bw. Julius Mosi.



Kulia ni baadhi ya watu waliokuwa katika Ibada.

# Mkuu awaonya manabii wa uongo

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ameshauri wakristo wajifunze vizuri Neno la Mungu ili *wasipeperushwe na kila upepo* kutoka *wachungaji ambao ni manabii wa uongo*.

Katika hotuba ambayo ilikuwa sehemu ya itikio lake baada ya kuingizwa kazini kuwa Mkuu wa KKKT katika Ibada iliyofanyika Kanisa Kuu la Kilutheri Moshi Mjini 31 Jan 2016, Askofu Dkt. Freidrick Shoo, alisema wachungaji kama hao wamebaki kujitajirisha binafsi na kuwaacha 'kondoo wakihangaika na hali zao zinabaki kuwa mbaya zaidi ya ilivyokuwa.'

Hivyo ni kinyume cha lengo la kukabidhiwa *'kundi la kondoo'* walichunge ili kutatua matatizo yao ya kiroho, kiakili na kimwili, alisema.

Manabii hao wamewageuza washarika kuwa kama 'mabuzi wa kuchuna' - yaani kama mtaji wao wa kupata fedha. Alisema 'wakati umefika kila mtu ashiriki kupiga vita ubinafsi uliokithiri katika jamii'.

## Wanasiasa waaswa

Mkuu wa KKKT pia alitaka wanasiasa wakiwa Bungeni wawe na heshima na kutumia lugha ya staha ili wawe mfano wa kuigwa kwa vizazi vijazo na kutunza heshima waliyonayo mbele ya jamii.

Ibada siku hiyo ilianza kwa maandamano yaliyoanzia Hosteli ya Umoja na baada ya Ibada wageni walialikwa katika hafla fupi ya chakula cha mchana katika Hoteli ya Uhuru ambayo ni mali ya Dayosisi ya Kaskazini.



**Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akisalimiana na mke wa Mkuu wa KKKT. Viongozi wengi wa kiroho, kijamii na wanasiasa walihudhuria Ibada.**



**Kanisa lihakikishe vituo vyake vya huduma za kijamii vitumike kufundisha watu maadili, haki na amani kwa ustawi wa jamii.**



**Wakuu wa KKKT kutoka kushoto: Askofu Dkt. Alex Malasusa (Awamu ya Nne), Askofu Dkt. Fredick Shoo (Awamu ya Tano) na Askofu Dkt. Samson Mushemba (Awamu ya Tatu).** (Picha na Jari Berg/ FELM).



**Washarika na viongozi wa Kanisa wakisikiliza mahubiri yaliyosisitiza kwamba Kanisa halina budi kutafuta 'kondoo' waliopotea na kuwarudisha kundini.**



**Tumtegemee Mungu na kushirikiana na wengine ili kufanikiwa na tusizitegemee akili zetu tu.**

## Malasusa aaga

Mkuu wa KKKT aliyemaliza muda wake, Askofu Dkt. Alex Gehaz Malasusa, alimshukuru Mungu, Kanisa, viongozi na Washarika wote kwa kumpa ushirikiano alipokuwa Mkuu wa KKKT kwa miaka minane.

Alisema alikuwa akiomba Mungu amwongoze hatua zake zote. Japo kazi ilikuwa ngumu; ni nguvu hiyo iliyomfanikisha, alisema.

Alimshauri Mkuu mpya awe mtu wa maombi ili Mungu amwongoze na asizitegemee tu akili zake mwenyewe bali aombe ushauri toka kwa watu wengine.



**Mchg. Dkt. Martin Junge, Katibu Mkuu wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) akihubiri siku ya kuingizwa kazini Askofu Dkt. Fredrick Shoo kuwa Mkuu wa KKKT 31 Januari 2016. Kushoto ni Mchg. Dkt. Rose Materu akimsaidia kutafsiri kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili.**

# Kuingizwa kazini ni hitaji la Katiba ya KKKT



**Baadhi ya maaskofu waliohudhuia Ibada wakiandamana kuingia kanisani.**

Mnapo waona Wakuu wa Dayosisi wakihudhuria kwa wingi katika Ibada ya kumwingiza kazini Mkuu wa Kanisa ni kwa kuwa ni hitaji la Katiba. Nukuu ya Katiba ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Toleo la 2011 inasema:

"Mkuu wa Kanisa ataingizwa kazini na Mkuu wa Kanisa aliyemtangulia au na Mkuu mmoja wapo wa Dayosisi atakayechaguliwa na Halmashauri Kuu, akishirikiana na Wakuu wengine wa Dayosisi wasiopungua nusu ya wote (50%). Siku ya kuingizwa kazini Mkuu wa Kanisa, maombi maalumu yatafanywa katika Kanisa zima kwa kusudi hilo. Dayosisi zitawakilishwa kwenye Ibada ya kumwingiza kazini Mkuu wa Kanisa."

Pia Katiba ya KKKT inataka Mkuu wa Kanisa achaguliwe kutoka miongoni mwa maaskofu wa KKKT. Na hutumika na Kanisa kwa sehemu ya wakati (part time) huku akitumika pia na Dayosisi yake.



**Baadhi ya watu wazima, vijana na watoto waliohudhuria Ibada.**



**Baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Maandalizi.**

# Dayosisi ya Kaskazini inakaribia kupanda miti milioni mbili



Bw. Julius Mosi,
Katibu Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini.

**Na Elizabeth Lobulu**

Uongozi wa Dayosisi ya Kaskazini kama zilivyo Dayosisi nyingine za Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) baada ya kushuhudia athari mbaya za uharibifu wa mazingira: ukame, mafuriko, ardhi kukosa rutuba kwa mmomonyoko wa udongo na mabadiliko ya tabia nchi, imeingia kwa nguvu katika kampeni ya kupambana na ukataji miti hovyo na kuhifadhi uumbaji.

Katibu Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini, Bw. Julius Mosi, alisema hivi karibuni kwamba kati ya mwaka 1997 na 2016 Dayosisi imefanikiwa kupanda miti 1,978,112 na ufikapo mwaka 2020 lengo ni kufikisha miti 3,237,400.

Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Shoo, ambaye pia ni Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini, amejizolea umaarufu ndani na nje ya nchi kwa kuhamasisha upandaji miti tangu akiwa Msaidizi wa Askofu katika dayosisi hiyo ya Kaskazini.

Alisema hivi karibuni kwamba jitihada hizo za kunusuru mazingira ni kutimiza wajibu wa kiroho na kwa sababu yeye anapenda mazingira na uumbaji wa Mungu. Alisema inapasa kutunza uumbaji wa Mungu jambo ambalo alilirudia Katibu Mkuu wa Dayosisi hiyo, Bw Julius Mosi, alipofafanua kwamba mbinu kubwa inayotumika ni kuhakikisha suala la mazingira ni mtambuka; hivyo kila idara na kila tukio lazima liambatane na jambo la mazingira.

Alisema katika miaka ya 60 na kurudi nyuma jitihada za makusudi zilikuwepo kuhakikisha watu wanatumia kilimo cha matuta na kujenga kingo kwenye mitelemko ya Mlima Kilimanjaro lakini kwa kiasi kikubwa jambo hili halizingatiwi na watu wengi kwa sasa. Bw. Mosi alisema wakati umefika sasa ambapo kila kitengo, idara na wizara zote zinazohusika na mazingira zianze kupanda miti badala ya kuendelea kutoa elimu au semina elekezi. Pia katika miji yote nchini miti ipandwe kando mwa barabara ili baada ya muda mfupi tupate miji iliyo ndani ya misitu, alisisitiza.

Naye Mratibu wa Mazingira ambaye pia ni Katibu wa Idara ya Wanawake Dayosisi ya Kaskazini, Mchg. Faustine Kahwa, alisema vikundi mbalimbali kama sharika, vijana, wanawake, shule na wanafunzi wa Kipaimara wamehimizwa kupanda miti. Katika kutekeleza kampeni hiyo, elimu ilitolewa kwa wahamasishaji (TOT) na fedha za kuanzisha vitalu vya miche zilitolewa na Dayosisi ili watu wengi waunge mkono jitihada za kutunza uumbaji.

Vijana wa kipaimara kwa kawaida hupangiwa kupanda mti mmoja usharikani au kanisani na miti miwili nyumbani.

Pamoja na Dayosisi kutumia makundi yake, mwaka 2014 ilipanua wigo kwa kuanzisha mtandao katika Ukanda wa Kaskazini uitwao NEFAT – 'Network of Faith on Environment Action in Tanzania' unaojumuisha wakristo na waislamu. Mchg. Kahwa alisema kupitia mtandao huo baadhi ya Shule za Sekondai za Kiislamu na za Kikiristo zimesaidiwa kupanda miti na kuanzisha vitalu vya miche ya miti.



Mchg. Faustiine Kahwa, Katibu wa Idara ya Wanawake na Mratibu wa Mazingira KKKT Dayosisi ya Kaskazini.

Alisema mwelekeo wa kampeni kwa sasa ni kuelekeza nguvu maeneo ya mijini na maeneo ya tambarare ambayo yamepata athari zaidi za uharibifu wa mazingira kuliko milimani ambako kwa sasa kasi ya kupanda miti inaridhisha.



Dayosisi ya Kaskazini ilianzisha Bustani ya maonesho karibu na Hoteli ya Uhuru, Moshi. Ina miti ya asili na ya kawaida. Viongozi wengi wa Kanisa na Serikali wamepanda miti eneo hilo.

# Dondoo muhimu za kutunza mazingira

**Na Patricia Mwaikenda**

Kuna mambo madogo ambayo kila mtu mahali alipo anaweza kufanya ili kuwa na mazingira rafiki au kuyatunza.

Endapo unaweza kupata maji ya bomba ofisini au nyumbani ukikuta bomba linatiririsha maji popote lifunge. Bomba likidondosha tone moja moja la maji hatimaye ndoo nzima inajaa baada ya muda. Pia funga bomba hasa wakati wa kupaka sabuni vyombo, nguo au unapooga. Tukifunga au kutengeneza bomba lililoharibika tunatunza mazingira maana maji ni rasilimali inayoisha, ikipotea hairudi tena.

Unapokuwa ofisini au nyumbani zima taa ambazo huzihitaji. Pia unapotayarisha chakula huna haja ya kuwasha jiko bali liwashwe unapoanza kupika. Kuwa na tabia ya kuzima jiko kama halitumiki. Wapo watu ambao wanapotumia jiko la umeme kuchemsha maji hawazimi tena jiko hata kama maji yamechemka muda mrefu uliopita. Kwa njia hizo tutatunza uumbaji maana hazitahitajika rasilimali nyingi kutengeneza nishati. Punguza matumizi ya karatasi kadri inavyowezekana.



Patricia Mwaikenda,
Mratibu wa Programu ya Uhai na Mazingira, KKKT.

**Wasiliana na Mratibu kwa sms: 0754 479 998.**

# Jinsi ya kuepuka mawazo mgando

Je wewe ni mtu wa mawazo mengi yanayo kufanya kila mara ujiulize *"mimi nina shida gani maishani?"* Au *"kwa nini ninajitendea haya?"* Au kusema *"mimi ni mpumbavu",* au kujiona uko peke yako mwenye matatizo, au kusema *"najua sifanikiwi"* au *"hali hii mbaya itaendelea mpaka lini?"*

Akili zetu hazipendi tuwe na mawazo hasi kama hayo ambayo husababisha tuwe na mashaka, wasiwasi, hofu na mara nyingi ni mawazo hasi ndio yanayojirudia rudia. Mawazo yakijirudia sana ujue umefika wakati wa kufanya mabadiliko maana mwili wako umechoka na unataka ugeuke utatue hilo tatizo. Mawazo kama hayo ni sawa na kuwa na kijiwe ndani ya kiatu. Haitakuwa sawa kuliambia jiwe litoke au liache kukuumiza au kujenga uadui nalo. Bali maumivu yanayosababishwa na jiwe yanataka ufumbuzi.

Hatua ya kwanza ni kwa wewe kuamua kuacha suluhu za kujidanganya na ghiriba zinazokuacha ubaki katika mawazo mgando yanayokuacha ukiwa na ufukara kiakili. Siyo mawazo yanayo kufukarisha bali ni kule kujikuta huna mkakati wa maana wa kutatua tatizo ulilonalo.

Ufanye nini basi? Ukikuza mawazo hasi yatakuletea shida lakini unaweza kuchukua hatua ili jiwe litoke katika kiatu chako. Geuza mawazo hasi kwa kuchukua hatua chanya; kwa kuwa na mawazo yenye upeo mpana zaidi ya mahali ulipo; usiendelee kufanya yale ya zamani ambayo hayakukupeleka popote; ondokana na mawazo mgando yanayokupa hofu na kukubana ubaki katika desturi ile ile inayo kugandamiza; usikwepe au kuukimbia wajibu bali uutimize; timiza maono mapana zaidi ya maendeleo katika maisha yako. Usibaki kuwaza tu mambo yaliyo ya hovyo au mabaya. Maisha ni zaidi ya kusoma magazeti ya udaku, au kutazama mpira wa Arsenal au mitandao ya kijamii kama 'Facebook' na 'WhatsApp.'

Ni muhimu kuendelea kukumbatia mafanikio uliyoyapata na usitetereke tena kwa kurudia mawazo mgando yasiyokusaidia bali yanayo kukurudisha nyuma. **(Mwandishi anapatikana sms: 0759 281 038)**

# Asasi ya ushauri na ujasiriamali yapatikana Same

"Same Counseling Foundation" ni Asasi ya ushauri iliyopo Wilayani Same, Mkoani Kilimanjaro. Iko karibu na Kituo cha Afya cha Tumaini Same mjini.

Ofisi hii inatoa huduma za ushauri kwa watu wa jinsi zote. Inatoa huduma za semina mbalimbali zinazowahusisha wadau wa masuala ya kijamii ikiwa ni pamoja na Dawati la Jinsia Polisi. Pamoja na semina, asasi hiyo inatoa ushauri elekezi kwa masuala ya ndoa; kuhamasisha jamii itambue haki na nafasi katika kukabiliana na umaskini na unyanyasaji katika jamii; hutoa mafunzo kuhusu sheria, ujasiriamali na kutoa hifadhi ya muda kwa mabinti na wanawake katika nyumba salama ili kuwajengea uwezo kujisimamia na kuwa wa msaada wanaporudi kuungana tena na familia zao. Kwa maelezo zaidi wasiliana na Mratibu +255 759 618 422 Barua pepe samecounselling@gmail.com au mmaridiana38@gmail.com

# MALEZI: Urithi kwa kizazi kijacho

Mungu amekugawia kipawa cha kuwaongoza watoto. Mungu angeweza kabisa kuwafanya watoto wajitegemee katika makuzi yao tangu wanapozaliwa lakini hakufanya hivyo bali ameacha tuwasaidie.

Watoto wanahitaji sana kuongozwa na watu wazima. tunapaswa kuwasaidia kwa kuwa tayari tumepitia njia hiyo ambayo watapitia. Biblia inasema: ***"Mlee mtoto katika njia impasayo naye hata iacha mpaka atakapokuwa mzee"*** (Mithali 22:6).

Ukitaka kuogelea lazima uwe na mwalimu mzuri wa kukufundisha ili akuonyeshe hatari inayoweza kutokea hata kama kwako unadhani ni jambo jepesi tu. Atakuonya mambo ya kujiepusha na magumu yanayoweza kujitokeza katika unachotaka kufanya.

Hali kadhalika hata watoto wanahitaji hayo. Wanataka wajifunze kutokana na makosa uliyoyafanya na hata maumivu uliyowahi kuyapata. Wangeweza pia kujifunza kutokana na uzoefu wao lakini wataepuka maumivu mengi kwa kujifunza kutoka kwako. Ni busara na jambo jepesi na haraka ukijifunza kutoka uzoefu wa watu wengine.

Mungu asingependa upoteze kumbukumbu ya makosa na maumivu yako ya nyuma bali anapenda uutumie kusaidia wengine. Unapokuta watu wanaelekea katika njia ambayo unafahamu ni hatari kwao sema nao. Huo ni upendo mkuu utakaoonesha kwa watu hao. Hata kama wewe si mzazi, watoto wanakuhitaji wewe katika maisha yao, na hata wewe unawahitaji!

Watoto wanatufundisha umuhimu wa kuwajali wengine na kutokuwa wabinafsi sana. Utawafundisha, lakini na wao pia watakufundisha mambo mengi. Kwa mfano, unaweza kuwafundisha kushinda majaribu kwa kujizuia na wao watakufundisha kufanya mambo kwa hiari toka moyoni na ubunifu. Je kwa sasa kuna watoto ambao si wako lakini unawasaidia?

## BARUA YA MSOMAJI

# Wito unatolewa elimu na siasa visichanganywe

Kila mara watu wameongea mambo mengi kuhusu uboreshaji wa elimu Tanzania lakini tatizo bado linaendelea kujitokeza kila siku.

Kutokana na baadhi ya viongozi wa kisiasa kutaka kujipatia umaarufu kupitia mwavuli wa Sekta ya Elimu ndiyo maana kila leo kiwango cha elimu kinazidi kushuka.

Hatuwezi kushindana na nchi kama Kenya na nchi nyinginezo za Afrika.

Tukitaka kufanikiwa katika elimu tuache kutafuta umaarufu wa kisiasa kupitia elimu.

Leo utakuta mtu amesoma hadi anafika ngazi ya chuo kikuu kwa njia ambazo zinaonekana ni nguzo ya siasa imembeba; je mnategemea tutaijenga Tanzania kwa mtindo huu?

**Anzawe Joshua Makweta**
**Chuo Kikuu cha Sokoine**

**Simu 0689 406 776**

**<13anzawemakweta@gmail.com>**

# Kamati ya Utendaji yakutana Arusha



Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Halmashari Kuu ya KKKT walikutana Arusha 16 Machi 2016 kwa mara ya kwanza tangu Mkuu wa Kanisa, Askofu Dkt. Fredrick Shoo (wa tano kutoka kulia), aingizwe kazini. Kulia kwake ni Katibu Mkuu wa KKKT, Bw.Brighton Killewa.

## Mkuu apokea ugeni wa Kanisa la Kongo



Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Shoo (wa tatu kutoka kushoto), alikutana na ujumbe wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Kongo (KKK-Kongo) katika Ofisi Kuu ya KKKT, Arusha mnamo 17 Machi 2016. Mkuu wa KKK-Kongo, Askofu Mwamba Sumaili (wa nne kutoka kushoto), aliongoza ujumbe huo akifuatana na Askofu Nawej Musehenu wa Dayosisi ya Kivu Kaskazini na Katibu Mkuu wa KKK-Kongo, Bw. Gilbet Ilunga Nkasa Talwa. Mazungumzo hayo yalihudhuriwa pia na Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa (wa pili kutoka kushoto) na Manaibu wote wanne kama ifuatavyo: Bw. Loata Mungaya, Mchg. Lazaro Rohho, Mchg. Rachel Axwesso na Bw. Mallumbo W. Mallumbo.

## Mmisionari Jari Berg aagwa



Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, akiagana na Mmisionari kutoka Finland (FELM), Bw. Jari Berg, alikuwa Mratibu wa Wamisionari wa FELM KKKT 2015 - 2016. Bw. Berg aliwahi kuwa mwakilishi wa FELM 2006 hadi 2008. Katika hafla fupi iliyofanyika Ofisi Kuu ya KKKT 26 Feb. 2016, Bw. Killewa alimwomba awe balozi wa KKKT na kumtakia heri na baraka za Mungu katika kazi yake mpya atakayofanya ya kuhudumia wakimbizi nchini Finland.

## Ugeni wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Bavaria



Naibu Katibu Mkuu Fedha na Utawala KKKT, Bw. Loata Mungaya (wa pili kutoka kulia), hivi karibuni aliongoza mazungumzo na wageni toka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Bavaria, Ujerumani. Kutoka kushoto ni Mchg. R. Hansen (Bavaria), Bw. Mallumbo W. Mallumbo (KKKT); Mchg. Rachel Axwesso (KKKT), Dkt. Gabrielle Hoescalmann (Bavaria) na Mchg. Manfred Scheckenbach (Bavaria).

## KKK-Marekani wachangia Mfuko wa wanawake



Kurugenzi ya Wanawake KKKT hivi karibuni ilipokea hati ya uthibisho wa ahadi ya Dola za Kimarekani 5,000 za kuanzisha 'Mfuko wa Kituo cha Wanawake KKKT'. Kituo kinatarajiwa kujengwa Wilaya ya Bahi, Mkoani Dodoma. Bibi Patti Austin, Rais wa Wanawake wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani (KKK-Marekani) alitoa hati hiyo alipoongoza ujumbe wa wanawake 13 kukutana na Uongozi wa KKKT (Ofisi Kuu), na kufanya mazungumzo na Uongozi wa Wanawake KKKT. Picha ya pamoja ya wageni na wenyeji wao.

## Ugeni wa Kanisa la Sweden wafika KKKT



Ujumbe wa watu 13 kutoka Kanisa la Sweden ulitembelea KKKT hivi karibuni ukitokea kambi za wakimbizi za Kenya na Ethiopia. Ujumbe huo ulitembelea wakulima wanaonufaika na Programu ya Uhai na Mazingira unaopata uhisani toka Kanisa la Sweden. Pichani wageni hao wakipata tafsiri toka kwa Katibu wa Tanzania katika Kanisa la Sweden, Bw. Lennart Adreasson, walipotembelea wakulima katika Dayosisi ya Meru.

# Tambua maono yako

Na Shemeji Melayeki



Bw. Shemeji Melayeki.

**Maono sio ndoto za usiku**

Maono ni muhimu kwa maendeleo ya kiroho, kiakili na kimwili. Bila maono tunakosa maendeleo katika maeneo hayo. Kama huna maono huweze kupima mafanikio. Na ndio maana Biblia inasema: *watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa.*

Maono siyo ndoto japo mtu anaweza kupata maono katika ndoto kama Yusufu alipoota na kuona jinsi jamaa yake ikimsujudia. Inakupasa uwe mtu unayependa kutumia akili yako kufikiri cha kufanya maishani ndipo utapata maono ambayo ni picha iliyokamilika juu ya maisha yako.

Watu wenye maono ndio wanasifika kwa kugundua mambo mengi duniani. Maono yanakusaidia kuweka picha kuhusu hali itakavyokuwa siku zijazo.

Wafanyakazi katika maeneo yao ya kazi wanakuta kila mwajiri ameweka taswira (maono) na dhamira ya taasisi au shirika lake. Lakini jiulize je, wewe japo ni mwajiriwa, una maono yako binafsi kwa maendeleo ya familia na jamii?

**Ufanye nini kuwa na maono binafsi?**

Tafakari kwa makini kipawa ulichonacho kwa mfano kuna wanaopenda kusoma kwa nini usiwaze na kuandika vitabu? Au kwa wanaopenda kukutana na watu kuwatia moyo, kwa nini usiwaze uwezekano wa kuwa mshauri au mhamasishaji. Kama ni mwalimu anza kwa kufundisha watoto wa 'tuisheni' au kama una kauli nzuri ya biashara kwa nini usiuze vitu vidogo vidogo au kufuga mifugo midogo, nk. Mambo kama haya unaweza kufanya wakati wa mapumziko au ukitoka kazini kama ni mwajiriwa. Uchague kitu unachokipenda au unachomudu kukifanya vizuri ndipo ukifanye.

Mtu asiye na maono yake atatumikia watu wengine walio na maono. Na si sawa kungoja hadi uzeeni ndipo uanze kujifunza kazi mpya au biashara mpya. Furahia maisha tangu sasa kwa kipato kitakachotokana na kutekeleza maono yako ya siku zijazo.

**Mtangulize Mungu akupe maarifa**

Ukisha mwomba Mungu akupe maono ya unachotaka kufanya kwa maendeleo ya familia au jamii; kaa chini tafakari zaidi na uandike maono hayo kwa kirefu.

Hata mtoto mdogo anapoanza shule anaanza kwa kuandika hewani na hata chini ardhini ili asisahau. Hivyo mawazo yako kuhusu maono yaandikwe ili umwombe Bwana akufanikishe kwa ile picha unayoiona mbele yako. Fanya kwa imani. Ukitaka kujenga nyumba unafikiria matumizi yake na ndipo unamwita mtu wa kukuchorea ramani. Mchoro unakusaidia kujiandaa kutekeleza. Baada ya hapo unachunguza gharama, namna ya kujenga, nini kianze, muda gani utatumika, nk. Na maono yatafikiwa kwa hatua kama hizo.

Maono yako yataongoza mwelekeo, hatua na hata kasi yako. Bila maono ni kama mtu asiyejua aendako kwa hiyo kwenda kokote ni sawa kwake. Ukitaka ufanikiwe katika maono upingane na nguvu inayokwenda kinyume na uendako. Pingana na jinsi ya dunia inavyokwenda.

Mtu aliye na maono anajua ashirikiane na nani kukamilisha maono aliyonayo. Atafanya uchaguzi sahihi, anajua kujizuia, vitabu gani asome au ahudhurie mafunzo ya aina gani.

Binadamu ameumbwa kwa kusudi la kumtumikia na kumpenda Mungu na wanadamu. Inampasa kusaidia maisha ya watu wengine. Hivyo angalia zaidi huduma gani ufanye ili kumsaidia mwanadamu mwingine kuliko kuangalia tu faida gani utapata ukitekeleza maono yako. Katika huduma kutoa huduma ndipo na wewe utanufaika.

Wapo watu wengi wamekuwa na muda wa kutafakari na wanafahamu maono yao lakini hawachukui hatua yo yote ya utekelezaji ili kufikia maono yao. Baadhi wana hofu kwamba watashindwa. Wengine wanaona uvivu kujibidiisha hivyo kubaki maskini. Usipokuwa na maono maisha yanakuwa hayana maana sana unakuwa kama mtu anayefukuza upepo. Hata hivyo watu wengine wanashindwa kwa kuwa wanaiga maono ya wengine na hivyo kushindwa kuyatekeleza.

**Hatua za kutekeleza kufikia maono**

Cha msingi ukipata maono anza kidogo na ulichonacho hadi baadaye utanue himaya yako hata dunia nzima. Anza kwa 'kuchimba msingi' kama ujenzi wa nyumba. Unapoanza upange kwamba utafanikiwa sana. Bila maono humpendezi Mungu. Mtu mwenye maono anajua pa kuelekeza nguvu zake na siyo kuondoka kwenye malengo ya maisha kwa kukubaliana na kila wazo.

**Bw. Shemeji Melayeki ni mwandishi wa vitabu. Wasiliana naye sms: 0763 965 297**

**Maburudiko ya Watumishi**

Watumishi wa Ofisi Kuu ya KKKT walikuwa na Siku ya Maburudisho Desemba 2015 ambapo walijadili mada mbili: Ya kwanza ilihusu "Maono" na ya pili ni kuhusu "Ugonjwa wa Saratani".

Pia walipata nafasi ya burudani - mashindano ya kuruka kamba, kukimbiza kuku, kupiga 'push up', nk.



**Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa (mwenye jezi nyekundu) akijiandaa kupiga dana dana ili kuanzisha kipindi cha burudani.**

# MAHUBIRI:

**Luka 15: 2 - 7**

# Kanisa lisimwache ye yote nyuma


**Na Mchg. Dkt. Martin Junge, Katibu Mkuu wa Fungamano la Makisa ya Kilutheri Duniani.**

Bwana Yesu alipokuwa akitoa huduma aliwaendea watu jinsi walivyokuwa na pale walipoishi - dini zao na maeneo yao, aliwatambua aliokutana nao na hakumwacha hata mmoja nyuma. Kwa sababu hiyo wapo waliosema kwamba anakula na wenye dhambi na kuwatembelea.

Kanisa leo linaitwa lisiache hata 'kondoo mmoja nyuma'. Somo kutoka Luka 15: 2-7 linahusu habari ya 'kondoo aliyepotea'. Kanisa linapewa wito kwamba lisimwache hata mtu mmoja nyuma bali limtafute kama kondoo mmoja aliyepotea kati ya kondoo 100 na mchungaji akawaacha wale 99 nyikani na kwenda kumtafuta yule mmoja aliyepotea na kumrudisha kundini.

Yesu alipokuja duniani alidhihirisha kwamba ni Mungu kweli na binadamu kweli. Na katika kueneza Neno alitumia mifano iliyokuwa rahisi kueleweka katika jamii aliyoihudumia.

Tunaona katika mfano huu: Jambo la kwanza kuna kundi lililotawanyika na mmoja kabaki nyuma. Pili ni kama vile Yesu anatukumbusha kuhusu wagonjwa katika jamii yetu; na watu waliovunjika moyo na jamii isiyo na umoja. Mwisho mfano huu unaeleza kuhusu mwana mpotevu ambapo kuna ambao hawakufurahi alipopokelewa kwa shangwe baada ya kurudi nyumbani kwa baba yake. Hii inatufundisha kwamba hata wale ambao hawafurahii kitendo cha aliyepotea kurudi kundini na wao



**Katibu Mkuu wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani, Mchg. Dkt. Martin Junge, akimkabidhi zawadi Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredick Onael Shoo.**

pia wamepotea.

Changamoto ya leo ni kwa watu kutengwa kutokana kwa kutotendewa haki kutokana na mabadiliko ya tabia nchi; kuongezeka kwa ufa kati ya matajiri na maskini na machafuko ambapo kanisa katika mahali tulipo na kimataifa linapaswa kuchukua hatua na kutoa kauli kuhusu uonevu kama huo.

Kutenga ni dalili za kukosa uadilifu. Umoja wenu (KKKT) na namna yenu ya kutatua tofauti miongoni mwenu ni kipawa chema kwa watu wenu.

Mnavyotembea, kushuhudia na kuhudumia jamii kwa pamoja ni mambo muhimu yanayo fahamika hadi nje ya mipaka ya kanisa.

Kiini cha ujumbe huu ni kwamba Mungu ni mwingi wa rehema, huruma tele na haki; sifa ambazo wanadamu hatuna. Neema ya Mungu kumkomboa mwanadamu haitokani na uwezo tulionao bali inatokana na asili ya Mungu alivyo.

Hivyo tuige mafundisho yake Yesu kwa kuhakikisha hakuna atakayepotea na hatumbakizi hata mtu mmoja nyuma.

Tuache mtazamo wa kuwabagua wenzetu; tuwakaribishe kama Kanisa kwa kutoa huduma za kijamii kwa mfano kuwasaidia wanaohitaji chakula, nk.

KKKT kwa kupitia Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Tanzania (TCRS), linanalo hisaniwa na FMKD, linahudumia maelfu ya wakimbizi kutoka Burundi. Pongezi KKKT kwa kutoa huduma hiyo kwa niaba ya makanisa 145 ya FMKD. Mfano huu uigwe na Kanisa kwa ujumla popote lilipo kwa kuendelea kutangaza Injili na kutoa huduma za kijamii na udikonia kwa watu wanaoteseka katika jamii na katika makanisa. Hii ni kuishi kwa vitendo wito wa kutoacha wengine bali kuwakubali na kuwashirikisha. Tunashukuru Kanisa kwa kampeni ya kupanda miti ili kuhifadhi mazingira. Askofu Dkt. Fredrick Shoo anafahamika kama "Askofu wa Miti" kwa kujitoa kwake katika kampeni ya upandaji miti. Kati ya mwaka 1997 na 2016 Dayosisi imepanda miti 1,978,112 na lengo ni kufika miti 3,237,400 ifikapo 2020.

Kanisa linahitaji kutoa sauti yake ya unabii kujenga umoja na kuingilia kati pale haki inapokosekana na kusababisha faraka na kubaguliwa na jamii badala ya kuwajengea watu matumaini. Watu wanahitaji kuona alama ya matumaini wakitazama milima kupata matumanini na kutiwa moyo na kuachana na magomvi na kukubali kutofautiana kwa njia ya amani.





# Sheria zinazopalilia unyanyasaji wa kijinsia

**Na Dkt. Helen Kijo-Bisimba**

Ukatili wa kijinsia sio dhana iliyofahamika na kutumika katika sheria au hata katika sera za nchi mbali mbali. Hii ni dhana ambayo kwa mara ya kwanza ilipata tafsiri rasmi katika Tamko la mwaka 1993 la Umoja wa Mataifa la "Ukomeshaji wa Ukatili Dhidi ya Wanawake".

Nchini Tanzania kuna hali ya wazi ya kutokuwa na usawa kati ya wanawake na wanaume kuanzia ngazi ya familia. Zipo Sheria nchini zinazoonekana kuvumilia ukatili wa kijinsia pamoja na kuwa Katiba inaweka bayana kuwa hakuna mtu yeyote atakayebaguliwa kwa sababu yoyote.

Ibara ya 13 inasema: Watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki, bila ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria. Ibara hii ina maana kuwa sheria zilizopo zinatakiwa kutoa huo ulinzi kwa kila mmoja vinginevyo sheria hizo zinakiuka Katiba.

**SHERIA ZA TANZANIA ZINAZOKINZANA**

Sheria zinazokiuka ibara hii na pia mikataba ya kimataifa tuliyoiridhia ni pamoja na Sheria inayojulikana kwa Kiingereza kama: "The Judicature and Application of Laws Act".

Katika Sura ya 358 ya Sheria iliyotajwa na kama ilivyorejewa mwaka 2002, inaruhusu sheria za Kimila za Makabila mbali mbali hapa Tanzania kutumiwa kama sheria za nchi.

Jedwali la kwanza la sheria hii linatambua sheria iitwayo "Sheria ya Hali ya Watu ya mwaka 1963" ikiwa ni sheria ya kimila ambayo hutumika katika Mahakama za Mwanzo. Katika sheria hii magomvi na vipigo hata kuumizwa katika ndoa vimeelezewa kwa njia ambayo si ya kutoa ulinzi bali ya kuvumilia hali hizo. Pia sheria hii inatambua mahari ambayo kwa upande mwingine inachochea ukatili wa kijinsia. Kwa mujibu wa sheria hii: "Mahari ni malipo ya ng'ombe au mali ya namna nyingine yalipwayo na bwana arusi kwa baba ya binti au mdhamini wake, sababu anataka kumwoa binti yake." Kifungu cha 37 "A" kinaeleza: "Baba wa binti au mrithi wake anaweza kutakiwa kurudisha mahari wakati ndoa inapovunjika." Na kifungu cha 37 "B" kinasema: "Mtu anayeweza kudaiwa kurudisha mahari ni yule aliyepokea mahari au mrithi wake." Ushahidi uliopo kwamba katika utekelezaji wa vifungu hivi mwanawake huonekana kama mali ya mume kwa vile mlipa mahari huwa na usemi mkubwa sana kwa mke aliyelipiwa mahari. Pia suala la mahari kurudishwa limewafanya wanawake wengi kubaki katika hali ya ukatili kwa vile wazazi waliopokea mahari hawako tayari kurudisha mahari na kwa hiyo inabidi mke yule avumilie tu. Hali hii imesababisha wanawake wengi kuteseka hata kufa kwa vile hawana mahali pa kwenda.



**Dkt. Helen Kijo-Bisimba, Mkurugenzi Mtendaji Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.**

Waliochukua mahari husumbuliwa na hata kufikishwa mahakamani wakidaiwa mahari; jambo linalowafanya wanawake walioachika kujisikia vibaya na hivyo wengi hubaki katika ndoa kwa vile hawana jinsi. Sheria ina vifungu vya kibaguzi ambavyo vinajenga hali ya kuendeleza ukatili kwa wanawake hasa ukatili wa kisaikolojia. Kwa mfano kifungu cha 106 kinaeleza kuwa 'Ugoni' wa mke ni sababu kwa talaka. Lakini kifungu cha 157 'A' cha sheria hii kinasema kuwa kwa kawaida za mila ugoni wa mume haufikiriwi sababu ya kuachana. Hivyo hata kama mke amemkamata mume wake kwa ugoni ataendelea kuishi naye tu kwa maumivu na msongo wa mawazo. Hali hii inaweza kuchangia katika kuwaumiza wanawake kisaikolojia pale ambapo mume anafanya vitendo vya ugoni na mke akakosa ulinzi kisheria.

"Sheria ya Hali ya Watu" inatambua na kuridhia aina ya ukatili dhidi ya wanawake unaofanywa na mume kama ilivyo katika kifungu cha 164 kuwa: Matendo ya nguvu kama kupigwa makofi au ngumi, kupiga kwa fimbo (hata kama kutia machubuko au uvimbe), kusukuma, kupiga mateke, kumtupia mke vitu vya nyumbani: Mambo hayo hayafikiriwi kuwa ni sababu za kuachana. Matendo hayo yanaonekana ni ya kawaida pamoja na kuwa kuna ushahidi wa wanawake kupoteza maisha kutokana na vitendo hivyo ndani ya ndoa zao. Kitu sheria hii inachofanya ni kujaribu kutoa adhabu kama vile fidia kwa mujibu wa kifungu cha 167. Kipimo cha fidia kina hitilafiana. Kwa mfano: Mapigano, michapo, kuvunjika kidole, kupoteza/ kuvunjika jino, jeraha dogo ambalo limepona kabisa - fidia yake katika kifungu "A" kinasema si chini ya shilingi kumi wala haizidi shilingi mia. Kifungu "B" kinasema : Kupiga mara kwa mara, kuvunja mguu au mkono ambao unaweza kuponeshwa - fidia yake si chini ya sh. 100/- na wala haizidi sh. 100/. Kifungu "C" kinasema: Madhara ya daima kwenye jicho, kuharibu kiungo daima, kupoteza sehemu ya nje ya sikio, kuharibu sura maisha - fidia yake si chini ya sh. 200/- na wala haizidi sh. 500/-.

Inapotokea kuwa kilema ni kibaya sana baraza linaweza kutoa amri kwamba mume baada ya kumuacha mkewe anabaki na wajibu wa kumtunza yule bibi mpaka kufa kwake.

Sheria hii kwa kuweka viwango vya fidia ili kuruhusu mume kumuumiza mke hata kama vingekua vikubwa ni kuwa inaridhia hali hii.

Lakini cha kutisha zaidi ni kuwa iwapo mume atamuumiza mkewe kiasi cha kumpa kilema basi anaweza kumuacha pamoja na kuwa atabaki na wajibu wa kumtunza. Sheria hii imepitwa na wakati kabisa na bado iko katika vitabu vya sheria na inatumika hadi sasa katika mahakama zetu.

Jedwali la pili la Sheria hii ya "Judicature and Application of Laws" linahusu sheria za mirathi za kimila ambazo nazo zinakiuka kabisa haki za wanawake na zinaendekeza ukatili dhidi ya wanawake. Sheria hii haitambui kuwa wanawake wana uwezo wa kuwa na mali ya kurithisha na hivyo inazungumzia kuwa urithi utakua upande wa baba.

Hii sheria kwa kutomtambua mwanamke kama mwenye uwezo wa kuwa na mali huleta migogoro inayo sababisha wajane kufukuzwa au hata kunyang'anywa mali. Wajane hawana nafasi ya usimamizi wa mali ya mume aliyekufa hata kama wana uwezo wa kuzisimamia mali na wamekua wakizisimamia hata kabla ya mume kufa. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha sheria hii kuwa: Msimamizi wa kugawanya urithi ni kaka wa marehemu aliye mkubwa, au babaye, na kama kaka au baba hakuna, ni ndugu wa kiume mwingine akisaidiwa na baraza la ukoo. Kama hakuna ndugu wa kiume, asimamie ndugu wa kike.

Sheria hii inaweka msisitizo kuwa mjane hana fungu katika mali za mume jambo hili pia linachangia katika kunyanyasa wanawake kwa kuwa tu ni wanawake: "Mjane hana fungu lake katika urithi ikiwa marehemu aliacha jamaa na ukoo wake: fungu lake ni kutunzwa na watoto wake, jinsi alivyowatunza." Hiki kifungu kinachochea kabisa ukatili wa kijinsia kiuchumi kwa vile hapa mjane ataanza ghafla kuwa tegemezi na itategemea kuwa ana hao watoto na iwapo wapo tayari kumtunza au wana uwezo huo wa kumtunza. Sheria hii imegawa watoto wa marehemu kwa madaraja ya umri na jinsi. Warithi daraja la kwanza ni mtoto mkubwa wa marehemu na warithi daraja la pili ni watoto wa kiume wengine wote na daraja la tatu ni watoto wa kike ambao hupewa fungu dogo kuliko wanaume na kwa mujibu wa kifungu cha 31 kama aliyebaki ni mtoto pekee wa kike atarithi mali yote isipokua ardhi ya ukoo. Hii wataitafutia ndugu wa kiume. Huu ni ubaguzi ambao hujenga ukatili dhidi ya wanawake.

# FAHAMU HISTORIA FUPI YA KKKT

**Kila mwaka Washarika wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania hukumbuka Siku ya KKKT ambayo mwaka huu itakuwa tarehe 19 Juni 2016. Ifuatayo ni historia fupi kuonesha chimbuko la siku hiyo:**

### Vyama vilivyoeneza Ulutheri

Mwanzo wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanganyika (KKKT) kuwepo nchini ni mwaka 1887, Chama cha Misioni cha 'Berlin III' au 'Evangelical Missionary Society for East Africa' (EMS) kutoka Ujerumani kilipoanzisha kazi ya Injili Kigamboni, Dar es Salaam.

### Chama cha pili

Chama cha Misioni cha 'Berlin I', nacho kutoka Ujerumani, kiliingia Tanzania kikitokea Afrika ya Kusini na kuanza kazi Nyanda za Juu Kusini mwaka 1891 kilipoanzisha kituo au misheni sehemu iitwayo Ipagika au Pipagika (Wangemannshöhe) katika Dayosisi ya Konde (kwa sasa).

Mwaka 1890 Chama cha Berlin III kilichukua sura mpya baada ya kubadili sera yake na kujulikana kwa jina la Bethel au Misioni ya 'Bethel'. Misioni hii ikafika sehemu za Tanga na kuanza kazi eneo la Mbuyukenda.

Baadaye Misioni hii iliamua kufikisha Injili ya Kristo nje ya mipaka ya Tanganyika. Wamisionari hao walipanga kwenda Rwanda kupitia Bukoba. Walipofika Bukoba wakafungua kituo mwaka 1910.

### Chama cha Leipzig

Chama cha tatu kufika nchini Tanzania ni Chama cha Misioni cha Leipzig, nacho kutoka Ujerumani. Kiliingia nchini Tanganyika mwaka 1893 na kuanza kazi ya misioni Kaskazini mwa nchi sehemu ya Kidia, Old Moshi na baada ya muda mfupi, kwa kushauriwa na Mtawala wa Kijerumani, Carl Peters, wakahamia Nkwarungo - Machame.

Pamoja na vyama vilivyoanzisha Ulutheri Tanzania, kuna mchango mkubwa wa vyama vya misioni na makanisa toka Ulaya na Marekani tunayo endelea kushirikiana nayo kama: **COS, ELCB, FELM, DLM, DANMISSION, SEM, LMW, MEW, NLM, NMZ, BMW, UEM, VELKD, ELCA,** nk. Hakika Neno la Mungu linaendelea kufundishwa kwa upendo na kwa usahihi wakati wote huu.

### Vita za Dunia

Kanisa la Kilutheri nchini lilipita katika nyakati ngumu vipindi vya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia 1914 - 1918 na ya Pili 1939 - 1945. Chama cha Misioni Augustana kutoka Marekani pamoja na Walutheri kutoka nchi nyingine za Ulaya walitoa msaada sana wakati wamisionari wa Kijerumani walipoondoka.

### Makanisa Saba

Vyama vya misioni viliendelea na kazi ya Injili na makanisa saba ya Kilutheri yakaanzishwa maeneo mbalimbali nchini. Makanisa hayo mwaka 1948 yaliunda Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Tanganyika. Na tarehe 23 Juni 1963 makanisa yale saba yaliungana na kuunda Kanisa moja la **KKKT** na makanisa yakageuka kuwa Dayosisi/ Sinodi. Sinodi zikageuka kuwa Dayosisi na hadi 2016 KKKT ina Dayosisi 24.

### Uongozi na usimamizi

Chombo kikuu cha maamuzi KKKT ni Mkutano Mkuu ambao hufanyika kila baada ya miaka minne. Halmashauri Kuu ya KKKT hukutana mara mbili kwa mwaka kwa vikao vyake vya kawaida. Wajumbe wa vyombo vyote hivi wanawakilisha Dayosisi zote za KKKT.

### Kazi za Umoja

Kanisa lina vituo na Ofisi Kuu ya Kazi za Umoja (Common Work). Ofisi Kuu ya Kanisa inaongozwa na Katibu Mkuu. Ina idara zifuatazo: Misioni na Uinjilisti; Mipango na Maendeleo; Fedha na Utawala; Huduma za Jamii, Kazi za Wanawake na Watoto. Pia kuna Kitengo cha Ukaguzi. Kazi ya Ofisi Kuu ya KKKT ni pamoja na ***kuratibisha, kuwezesha na kufanya utetezi*** kwa manufaa ya Kanisa zima.

KKKT ina taasisi na vituo vinavyotunza Kazi za Umoja: **1.** Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira **2.** Seminari Ndogo ya Kilutheri Morogoro **3.** Kituo cha Redio Sauti ya Injili, Moshi. **4.** Shule za Msingi kwa watoto viziwi Mwanga na Njombe. **5.** Shule ya Sekondari kwa watoto viziwi Njombe. **6.** Miradi ya kuongeza kipato.

Pamoja na vituo vya Kazi za Umoja, Dayosisi zina hospitali 20 na zahanati / vituo vya afya 150. Dayosisi zote zina shule za msingi, sekondari na vyuo vya ufundi na maarifa mbalimbali. Baadhi ya Dayosisi zina vyuo vikuu. Taasisi hizi hutoa huduma kwa watu wote bila ubaguzi.

Karibu kila dayosisi /taasisi zake/ idara zina miradi midogo midogo ya kuinua kipato; miradi ya maji salama, miradi ya ng'ombe wa maziwa, nk. Dayosisi nyingi zina miradi mikubwa na ya kati. Baadhi zimeanzisha mabenki au vyama vikubwa vya kuweka na kukopa (SACCOs).

### Kazi za Misioni

KKKT inajihusisha na kazi za misioni ndani na nje ya Tanzania. Baadhi ya maeneo nje ya nchi ni Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Msumbiji, Malawi, Uganda na Zambia. Ndani ya nchi maeneo ya misioni ni Tabora, Kigoma na Zanzibar.

### Ushirikiano na wengine

KKKT ni mwanachama hai wa: Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT); 'Lutheran Mission Cooperation' (LMC); Baraza la Makanisa Barani Afrika (AACC); Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (LWF) na Baraza la Makanisa Duniani (WCC).

### Ofisi zilipo

Ofisi Kuu ya KKKT ipo Arusha "Lutheran Centre", Barabara ya Boma mkabala na Posta Kuu. Senta hiyo ina hosteli yenye vitanda 24 kwa ajili ya watumishi na wageni wa Kanisa.

### Kwa maelezo zaidi wasiliana na

**Katibu Mkuu**
Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania
**S.L.P.** 3033, **Arusha**
**Simu: 250 8856/ 250 8857**
**Fax** 254 8858
**Barua pepe:** elcthq@elct.or.tz

**Tovuti: http**//www.elct.org/
**Au: http**//www.elct.or.tz/

**Siku ya KKKT 19 Juni 2016: Tudumishe umoja wa Kanisa.**

# NEW SAFARI HOTEL (1967) LTD

establish since **1935**

P.O. Box 303, Phone +255 27 254 5940/1, F ax +255 27 254 8318

Arusha – TANZANIA. newsafarihotel@habari.co.tz - www.newsafarihotel.com





The Board, Management and Staff of New Safari Hotel congratulate the newly elected Bishop Dr. Fredrick O. Shoo as the 5th Presiding Bishop of Evangelical Lutheran Church in Tanzania (ELCT). The New Safari Hotel is privileged to commemorate with ELCT members on this important event, with

"Karibuni katika Hotel Yenu"

**for 2016**
**30% up to 50% OFF**
**FOR All ELCT Parishes Members**

# www.newsafarihotel.com